**TUME YA MABADILIKO YA KATIBA**

**Makao Makuu**

Mtaa wa Ohio, karibu na Wizara ya
Mambo ya Ndani ya Nchi
S.L.P 1681,
**DAR ES SALAAM.**

Simu: +255 22 2133425
Nukushi: +255 22 2133442

Au

**Ofisi Ndogo**

Jengo la Ofisi ya Mfuko wa Barabara,
Mtaa wa Kikwajuni Gofu,
S.L.P. 2775,
**ZANZIBAR**
Simu: +255 24 2230 768
Nukushi: +255 24 2230 769

*'Toa Maoni, Tupate Katiba Mpya'*

**Dira**

Kufanikisha  Kupatikana kwa Katiba Mpya

**Dhamira**

Kuratibu, Kukusanya na Kutathmini Maoni ya Wananchi ili Kupatikana Katiba Mpya

**Maadili Yetu Ya Msingi**

- *Uwajibikaji*
- *Uadilifu*
- *Usawa*
- *Uwazi na*
- *Uhuru katika kufanya kazi*

## ELIMU KUHUSU KATIBA YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA YA MWAKA 1977 (KWA LUGHA NYEPESI)

### UTANGULIZI

Chimbuko la mamlaka ya dola ni wananchi wenyewe. Serikali hupata uhalali wake kutokana na wananchi kupitia Katiba. Vilevile kushiriki kwa wananchi katika maamuzi kuhusu mambo yanayogusa maslahi yao ni msingi mkuu wa utawala wa ki-demokrasia. Kwa misingi hiyo, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iko katika mchakato wa kupata Katiba mpya. Kwa kuwa Katiba ni uamuzi wa wananchi jinsi wanavyotaka kuishi, kujiongoza na kuendesha nchi yao, mabadiliko ya Katiba yanawapatia Watanzania fursa kubwa ya kuzaliwa upya kikatiba, kisheria, kisiasa, kiuchumi na kijamii. Hii ndiyo sababu kubwa kwa nini Watanzania wote washiriki kikamilifu katika mchakato wa kujipatia Katiba Mpya. Serikali imeshaunda Tume ya Mabadiliko ya Katiba ambayo jukumu lake ni kuratibu mchakato wa maandalizi ya rasimu ya Katiba Mpya itakayotokana na ushiriki mpana wa wananchi kadri inavyowezekana.

Sheria ya Mabadiliko ya Katiba, Sura ya 83 Toleo la 2012, inaipa Tume jukumu la kuandaa na kuendesha programu za kuelimisha umma juu ya madhumuni na majukumu ya Tume. Jukumu kuu la Tume ni kukusanya maoni ya wananchi juu ya mabadiliko ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Jukumu hili ni kubwa na lazima litekelezwe kwa umakini mkubwa. Elimu ya umma kuhusu Katiba iliyopo ni ufunguo wa utekelezaji wa jukumu hili.

Kitabu hiki kinalenga kuwasilisha kwa kifupi maudhui ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama ilivyo sasa.

Kimeandikwa kwa lugha rahisi na kwa ufupi ili kujenga uelewa wa haraka kuhusu Katiba iliyopo. Msomaji anashauriwa akipenda kulinganisha maelezo yaliyomo na Katiba yenyewe kama anayo. Ikiwa hana, kitabu hiki kitatosha kumwezesha msomaji kujenga hoja kuhusu mambo kadha wa kadha yaliyo kwenye Katiba iliyopo.

## MPANGILIO WA KATIBA YA TANZANIA

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imegawanywa katika sura kumi kama ifuatavyo:

(i) Misingi ya katiba;

(ii) Jamhuri ya Muungano, vyama vya siasa, watu na siasa ya ujamaa na kujitegemea;

(iii) Serikali ya Jamhuri ya Muungano;

(iv) Bunge la Jamhuri ya Muungano;

(v) Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Baraza la Mapinduzi Zanzibar, na Baraza la Wawakilishi Zanzibar;

(vi) Utoaji haki katika Jamhuri ya Muungano, Mahakama Kuu ya Jamhuri ya Muungano, Tume ya Mahakama ya Tanzania Bara, Mahakama Kuu ya Zanzibar, Mahakama ya Rufani ya Jamhuri ya Muungano na Mahakama Maalumu ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano;

(vii) Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora na Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma;

(viii) Masharti Kuhusu fedha za Jamhuri ya Muungano;

(ix) Madaraka ya Umma;

(x) Majeshi ya Ulinzi;

(xi) Mengineyo.

## MAELEZO MAFUPI YA KILA SURA
## UTANGULIZI

### MISINGI YA KATIBA

**Misingi ya Katiba imetajwa kwenye utangulizi kama ifuatavyo:-**

*Kwa kuwa sisi Wananchi wa Jamhuri ya Mungano wa Tanzania tumeamua rasmi na kwa dhati kujenga katika nchi yetu jamii inayozingatia misingi ya uhuru, haki, udugu na amani:*

*Na kwa kuwa misingi hiyo yaweza tu kutekelezwa katika jamii yenye demokrasia, ambayo Serikali yake husimamiwa na Bunge lenye wajumbe waliochaguliwa na linalowawakilisha wananchi, na pia yenye Mahakama huru zinazotekeleza wajibu wa kutoa haki bila woga wala upendeleo wowote, na hivyo kuhakikisha kwamba haki zote za binadamu zinadumishwa na kulindwa, na wajibu wa kila mtu unatekelezwa kwa uaminifu:*

*Kwa hiyo basi, Katiba hii imetungwa na Bunge Maalum la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa niaba ya Wananchi, kwa madhumuni ya kujenga jamii kama hiyo, na pia kwa ajili ya kuhakikisha kwamba Tanzania inaongozwa na Serikali yenye kufuata misingi ya demokrasia, ujamaa na isiyokuwa na dini.*

Kutokana na utangulizi huu Katiba ya Jamhuri ya Muungano inataja misingi ya Taifa kuwa ni uhuru, haki, udugu na amani. Misingi hii inahitaji mazingira ya demokrasia inayozingatia uchaguzi huru na wa haki unaofanywa na wananchi kila kipindi kilichopangwa, Bunge huru lenye mamlaka ya kuiwajibisha Serikali na Mahakama huru zenye kutoa haki bila woga, upendeleo na rushwa na Serikali yenye kufuata misingi ya demokrasia na isiyofungamana na dini yoyote.



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mh. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, akiongea na Wajumbe na Sekretarieti ya Tume ya Mabadiliko ya Katiba alipotembelea Ofisi za Tume Jijini Dar es Salaam.

## SURA YA KWANZA

## JAMHURI YA MUUNGANO, VYAMA VYA SIASA, WATU NA SIASA YA UJAMAA NA KUJITEGEMEA.

### NCHI MOJA NA DOLA MOJA LA JAMHURI

Ibara ya kwanza ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano inaeleza kuwa Jamhuri ya Muungano ni nchi moja ambayo dola yake ni ya kijamhuri.

### MIPAKA

Ibara ya Pili ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano inaeleza kuwa mipaka na eneo la Jamhuri ya Muungano ni eneo lote la Tanzania Bara na eneo lote la Zanzibar ikijumuisha eneo la bahari.

### VYAMA VYA SIASA NA ITIKADI

Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano dola itaongozwa kwa misingi ya kidemokrasia kwa mfumo wa vyama vingi vya siasa na kuwa dola yenyewe haina dini na itafuata itikadi ya ujamaa na kujitegemea.

### MAMLAKA YA DOLA

Ibara ya 4(1) na (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano inagawanya mamlaka ya dola katika mihimili mitatu ya dola ya Jamhuri ya Muungano, kwa maana ya serikali mbili, ile ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, vyombo viwili vya kutunga sheria ambavyo ni Bunge la Jamhuri ya Muungano na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, na vyombo viwili vya kimahakama ambavyo ni Mahakama Kuu ya Jamhuri ya Muungano na Mahakama Kuu ya Zanzibar.

## MAMLAKA YA JAMHURI YA MUUNGANO

Ibara ya 4 (3), ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano inagawanya madaraka kati ya Zanzibar na Jamhuri ya Muungano. Mgawanyo huo umeorodhesha mambo 22 ya Muungano kama ifuatavyo:

(i) Katiba ya Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Muungano;

(ii) Mambo ya Nchi za Nje;

(iii) Ulinzi na Usalama;

(iv) Polisi;

(v) Mamlaka juu ya mambo yanayohusika na hali ya hatari;

(vi) Uraia;

(vii) Uhamiaji;

(viii) Mikopo na Biashara ya Nchi za Nje;

(ix) Utumishi katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano;

(x) Kodi ya mapato inayolipwa na watu binafsi na mashirika, ushuru wa forodha na ushuru wa bidhaa zinazotengenezwa nchini Tanzania unaosimamiwa na Idara ya Forodha;

(xi) Bandari, mambo yanayohusika na usafiri wa anga, posta na simu;

(xii) Mambo yanayohusika na sarafu na fedha kwa ajili ya malipo yote halali (pamoja na noti); mabenki (pamoja na

mabenki ya kuweka akiba) na shughuli zote za mabenki; fedha za kigeni na usimamizi juu ya mambo yanayohusika na fedha za kigeni;

(xiii) Leseni za viwanda na takwimu;

(xiv) Elimu ya juu;

(xv) Maliasili ya mafuta, pamoja na mafuta yasiyochujwa ya motokaa na mafuta aina ya petrol na aina nyinginezo za mafuta au bidhaa, na gesi asilia;

(xvi) Baraza la Taifa la Mitihani la Tanzania na mambo yote yanayohusika na kazi za Baraza hilo;

(xvii) Usafiri na usafirishaji wa anga;

(xviii) Utafiti;

(xix) Utabiri wa hali ya hewa;

(xx) Takwimu;

(xxi) Mahakama ya Rufani ya Jamhuri ya Muungano;

(xxii) Uandikishwaji wa Vyama vya Siasa na mambo mengine yanayohusiana nayo.

Mambo ya Muungano na mambo yote ya Tanzania Bara yako chini ya Serikali ya Muungano na mambo yote ya Zanzibar yasiyokuwa ya Muungano yako chini ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

## JAMHURI NA DEMOKRASIA

Katiba ya Jamhuri ya Muungano inampa kila raia mwenye umri wa miaka 18 haki ya kupiga kura katika uchaguzi unaofanywa na wananchi. Haki ya kupiga kura, daftari la kudumu la wapiga kura vimeainishwa katika sheria ya uchaguzi. Hivyo hakuna haki, hadhi au cheo maalumu kitakachoundwa katika Jamhuri ya Muungano kwa misingi ya nasaba, jadi au urithi.

## MALENGO MUHIMU YA TAIFA NA MISINGI YA MWELEKEO WA SHUGHULI ZA SERIKALI

Katiba ya Jamhuri ya Muungano inaweka Maadili ya Taifa na maamuru kuhusu sera za Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Kwa mujibu wa maelekezo hayo, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni nchi inayofuata misingi ya demokrasia na haki ya kijamii na kwa hiyo:

a) Wananchi ndiyo msingi wa mamlaka yote, na Serikali itapata madaraka na mamlaka yake yote kutoka kwa wanachi kwa mujibu wa Katiba;

b) Lengo kuu la Serikali litakuwa ni ustawi wa wananchi;

c) Serikali itawajibika kwa wananchi;

d) Wananchi watashiriki katika shughuli za Serikali kwa mujibu wa masharti ya Katiba;

Pia Katiba inaweka sharti kuwa katika muundo na uendeshaji wa shughuli zake, Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zitazingatia umoja wa Jamhuri ya Muungano

na haja ya kukuza umoja wa kitaifa na kudumisha heshima ya Taifa. Pia Katiba ya Jamhuri ya Muungano inataja wazi lengo lake kuwa ni kuwezesha ujenzi wa Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa misingi ya udugu, umoja na amani na kufuata siasa ya ujamaa na kujitegemea. Hivyo basi Serikali za Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zina jukumu la kuhakikisha kwamba:

a) Utu na haki nyinginezo zote za binadamu zinaheshimiwa na kuthaminiwa;

b) Sheria za nchi zinalindwa na kutekelezwa;

c) Shughuli za Serikali zinatekelezwa kwa njia ambazo zinahakikisha kwamba utajiri wa Taifa unaendelezwa, unahifadhiwa na unatumiwa kwa manufaa ya wananchi wote kwa ujumla na pia kuzuia mtu kumnyonya mtu mwingine;

d) Maendeleo ya Watanzania yanakuzwa na kupangwa kwa ulinganifu na kwa pamoja;

e) Mtu mwenye uwezo wa kufanya kazi anafanya kazi, na kazi maana yake ni shughuli yoyote ya halali inayompatia mtu riziki yake;

f) Heshima ya binadamu inahifadhiwa na kudumishwa kwa kufuata kanuni za Tangazo la Dunia Kuhusu Haki za Binadamu;

g) Serikali na vyombo vyake vyote vya umma vinatoa nafasi zilizo sawa kwa raia wote, wake kwa waume, bila ya kujali rangi, kabila, dini au hali ya mtu;

h) Aina zote za dhuluma, vitisho, ubaguzi, rushwa uonevu au upendeleo zinaondolewa nchini;

i) Matumizi ya utajiri wa taifa yanatilia mkazo maendelo ya wananchi na hasa zaidi yanaelekezwa kwenye jitahada ya kuondosha umaskini, ujinga na maradhi;

j) Shughuli za uchumi haziendeshwi kwa njia zinazoweza kusababisha ulimbikizaji wa mali au njia kuu za uchumi katika mamlaka ya watu wachache binafsi;

k) Kwamba nchi inatawaliwa kwa kufuata misingi ya demokrasia na ujamaa.

Katiba inaweka masharti ya kila mtu kujipatia elimu na kila mtu kufanya kazi na kujipatia riziki yake kwa njia halali.

## MALENGO NA MISINGI YA MWELEKEO WA SHUGHULI ZA SERIKALI

Katiba inawekea mipaka ya kuzuia uhimizaji kupitia mahakama wa utekelezaji wa maadili ya taifa na maamuru ya sera za Serikali. Hivyo hakuna mahakama yoyote nchini itakayokuwa na mamlaka ya kutoa hukumu, kuhimiza kutenda au kuadhibu kwa kutotekeleza lolole lililoelekezwa katika orodha hiyo kuanzia (a) hadi (k) na maelekezo mengine yaliyo kwenye Ibara ya 6 hadi 11 ya Katiba.

## HAKI ZA BINADAMU

Katiba ya Jamhuri ya Muungano imeweka, kulinda na kuziwekea mipaka haki za binadamu. Nyingi katika haki hizi zimepokelewa au kuasilishwa kwa kiasi kikubwa baadhi ya haki za binadamu zilizotangazwa kwenye Tangazo la Dunia Kuhusu Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa la mwaka 1948 na pia baadhi

ya haki zilizo kwenye Mkataba wa Afrika kuhusu Haki za Binadamu na za Watu za mwaka 1981. Haki zenyewe ni kama zifuatazo:

- Haki ya usawa wa binadamu na stahili ya kuheshimiwa na kuthaminiwa utu wa binadamu;
- Usawa mbele ya sheria na hivyo haki ya kusikilizwa kikamilifu mbele ya mahakama za sheria za nchi, haki hii ikiwa ni pamoja na haki ya kukata rufaa kwenye mahakama za rufani za nchi;
- Haki ya kutotendewa kama mhalifu kabla ya kupatikana na hatia na mahakama halali za nchi;
- Haki ya kutoadhibiwa bila kosa lililowekwa kisheria;
- Haki ya kutopewa adhabu isiyolingana na kosa, iliyopita kipimo au ya kudhalilisha;
- Haki ya kutobaguliwa kwa namna yoyote ile kijinsia, rangi, kabila au hali ya kimaisha;
- Haki ya kuishi;
- Haki ya faragha;
- Uhuru wa mtu kwenda atakako;
- Haki ya uhuru wa kuwa na mawazo na kuyaeleza kwa uhuru;
- Haki ya kuamini na kuabudu;

- Haki ya kushirikiana na wengine;
- Haki ya kushiriki katika mambo ya nchi kwa kuchagua na kuchaguliwa;
- Haki ya kufanya kazi na kupata ujira stahili n.k.

**MIPAKA YA HAKI ZA BINADAMU**

Katiba ya Jamhuri ya Muungano inaziwekea haki za binadamu mipaka hasa upatikanaji wake kupitia chombo cha mahakama kwanza kwa kuziondoshea mahakama madaraka ya kufuta sheria zinazopingana na haki za binadamu. Pili, Katiba inaziwekea baadhi ya haki za binadamu mipaka, kwa mfano haki ya kushiriki kwenye shughuli za nchi kwa kuchaguliwa kuwa kiongozi imewekewa mipaka hivyo kwamba lazima mtu awe mwanachama wa chama cha siasa na apendekezwe na chama chake kugombea nafasi ya uongozi wa kuchaguliwa. Pia katiba inaweka mipaka ya haki ya mtu binafsi kutotumika vibaya na kuathiri haki na uhuru wa watu wengine au maslahi ya umma. Vyama vya Siasa vimepewa pia madaraka ya kumvua mwanachama wake ubunge au udiwani.

## SURA YA PILI

## SERIKALI YA JAMHURI YA MUUNGANO

Serikali ni muhimili wa dola ambao unatekeleza maamuzi yaliyowekwa katika mfumo wa sheria. Serikali huundwa na Rais, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, Mawaziri na Manaibu Waziri. Chombo kikuu cha Serikali ni Baraza la Mawaziri ambalo lionaongozwa na Rais. Kiongozi Mkuu wa Jamhuri ya Muungano ni Rais ambaye ni mkuu wa dola, Serikali na Amiri Jeshi Mkuu wa Jamhuri ya Muungano. Serikali ya Jamhuri ya Muungano inayo mamlaka kuhusu mambo yote ya Jamhuri ya Muungano na pia mambo yote kuhusu Tanzania Bara.

## MADARAKA YA RAIS

Rais wa Jamhuri ya Muungano ndiye mtendaji mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano na anayo mamlaka yafuatayo:

- Kuunda na kufuta nafasi yoyote ya utumishi katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano;

- Kuwateua, kuwaondoa madarakani watendaji wakuu wafuatao:

  - Waziri Mkuu, ambaye lazima aidhinishwe na Bunge kwa kura ya Siri.

  - Mawaziri na Manaibu Waziri,

  - Mwanasheria Mkuu na Naibu Mwanasheria Mkuu,

  - Mkurugenzi wa Mashtaka,

- Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya,

- Wakuu wa Majeshi ya Ulinzi,

- Wakuu na Wajumbe wa Tume mbalimbali ikiwa ni pamoja na Tume ya Taifa ya Uchaguzi na Tume ya Haki za Binadamnu na Utawala Bora;

- Jaji Mkuu;

- Jaji Kiongozi na Majaji wa Mahakama Kuu kwa ushauri wa Tume ya Utumishi wa Mahakama;

- Majaji wa Rufaa kwa ushauri wa Jaji Mkuu;

Pia Rais husimamia nidhamu ya majaji na anayo mamlaka ya kumwondoa Jaji kwenye nafasi ya Ujaji kwa pendekezo la Jopo la Majaji watatu kutoka nchi za Jumuiya ya Madola. Pia uteuzi wa Waziri Mkuu ni lazima uthibitishwe na Bunge.

Rais ni sehemu ya kwanza ya Bunge la Jamhuri ya Muungano mwenye mamlaka ya kuweka saini kwenye Miswada ya sheria iliyopitishwa na Bunge kuwa sheria. Mamlaka mengine ya Rais ni yale ya kutoa msamaha kwa wafungwa. Pia ana mamlaka kutangaza hali ya hatari na vita, na kuwasilisha hati kwenye Bunge ili lipige kura ya kukubali au kukataa.

**MATUMIZI YA MAMLAKA YA RAIS**

Rais wa Jamhuri ya Muungano hutumia mamlaka yake kwa mujibu wa Katiba na Sheria za nchi. Hata hivyo Katiba inamruhusu Rais kutumia utashi wake mwenyewe kuchukua maamuzi ya kuiongoza nchi bila kufungwa na ushauri aliopata kutoka kwa mtu au mamlaka yoyote ile isipokuwa tu kama Katiba au sheria inamtaka afanye hivyo.

## SABABU ZA KUMWONDOA RAIS MADARAKANI

Katiba inaweka utaratibu wa kikatiba wa kumwondoa Rais madarakani endapo atakuwa hana uwezo tena wa kutekeleza majukumu yake kutokana na maradhi ya mwili au akili. Pia Katiba inaweka utaratibu wa kuhuisha madaraka kwa Makamu wa Rais au Waziri Mkuu itokeapo kuwa Rais hayupo nchini. Rais anaweza kuondolewa madarakani kwa kura ya Bunge ya kutokuwa na imani naye ikiwa atavunja Katiba, kukiuka maadili ya uongozi au kufanya vitendo vya kudhalilisha ofisi ya Rais. Kabla ya kupiga kura ya kumwondoa Rais madarakani lazima yatolewe mashitaka na Wabunge wasiopungua asilimia ishirini ya Wabunge wote. Baada ya hapo itaundwa Kamati yenye wajumbe tisa, ikiwa ni pamoja na Jaji Mkuu wa Jamhuri ya Muungano akiwa Mwenyekiti, Jaji Mkuu wa Zanzibar na wajumbe saba wa kuteuliwa na Spika.

## SIFA ZA KUCHAGULIWA RAIS

Sifa za kuchaguliwa kuwa Rais ni kama zifuatazo:

a) Kuwa raia wa kuzaliwa;

b) Kuwa na umri usiopungua miaka 40;

c) Kuwa mwanachama wa chama cha siasa na kupendekezwa na chama hicho kuwa mgombea;

d) Kuwa na sifa za kuchaguliwa kuwa mbunge au mjumbe wa Baraza la wawakilishi Zanzibar;

e) Kutokuwa na hatia ya kutolipa kodi ya Jamhuri ya Muungano katika kipindi kisichopungua miaka mitano kabla ya uchaguzi.

Tume ya Uchaguzi ikitangaza mgombea kwamba amechaguliwa kuwa Rais hakuna Mahakama itakayokuwa na mamlaka ya kuchunguza kuchaguliwa kwake.

**KIPINDI CHA URAIS**

Rais wa Jamhuri ya Muungano hushika cheo hicho kwa muda wa miaka mitano na anaweza kuchaguliwa tena kwa kipindi kingine kimoja tu.

**BARAZA LA MAWAZIRI**

Baraza la Mawaziri linateuliwa na Rais na ndicho chombo kikuu cha kumshauri Rais kuhusu utendaji wa Serikali. Waziri Mkuu ni kiongozi mwenye mamlaka ya kudhibiti na kusimamia utekelezaji wa majukumu wa kila siku wa Baraza la Mawaziri na yeye ndiye pia kiongozi wa shughuli za Serikali Bungeni. Waziri Mkuu huteuliwa na Rais kutokana na wabunge wa kuchaguliwa majimboni kutoka chama cha siasa chenye wabunge wengi.

**UWAJIBIKAJI WA MAWAZIRI BUNGENI**

Maamuzi yote ya sera za nchi hufanywa na Serikali kwa mujibu wa Katiba na hivyo Mawaziri wakiongozwa na Waziri Mkuu huwajibika kwa pamoja Bungeni juu ya utekelezaji wa sera hizo. Hii ina maana kuwa Bunge laweza kupitisha azimio la kutokuwa na imani ama na Waziri mmoja au Mawaziri wote na kwa jinsi hiyo kuwawajibisha kwa utendaji wao.

Bunge lina mamlaka ya kupitisha azimio la kutokuwa na imani na Waziri Mkuu kwa kupitisha azimio kwa wingi wa kura na kwa jinsi hiyo kumwondoa madarakani Waziri Mkuu.

## SURA YA TATU

## BUNGE LA JAMHURI YA MUUNGANO

Bunge la Jamhuri ya Muungano lina sehemu mbili yaani, Rais wa Jamhuri ya Muungano ambaye ni sehemu ya kwanza na Wabunge ambao ni sehemu ya pili. Sehemu hii ya pili inapofanya kazi zake bila kumhusisha Rais ndiyo kwa lugha ya kawaida huitwa Baraza la Taifa 'National Assembly'. Kwa maana hiyo, katika utekelezaji wa majukumu yake makuu, kama vile kutunga sheria, wajibu huo utatekelezwa kwa kila moja ya sehemu hizi mbili kutekeleza wajibu wake ndipo sheria itapatikana. Hivyo Wabunge watajadili na kupitisha muswada wa sheria na watauwasilisha Muswada huo kwa Rais ili aweke saini kuuridhia.

## MAJUKUMU YA BUNGE

Bunge kwa maana ya Baraza la Taifa lina majukumu yafuatayo:

(a) Kusimamia na kuishauri Serikali na vyombo vyake vyote kuhusu utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa Katiba.

(b) Kuihoji Serikali kuhusu utekelezaji wa wajibu wake kwa umma;

(c) Kujadili bajeti za Wizara na kujadili utekelezaji wa kila Wizara ya Serikali;

(d) Kujadili na kuidhinisha mipango ya maendeleo na kutunga sheria ya utekelezaji wa mipango hiyo;

(e) Kutunga sheria za Jamhuri ya Muungano na sheria za Tanzania Bara;

(f) Kujadili na kuridhia mikataba.

**AINA ZA WABUNGE**

Kwa mujibu wa Katiba, Bunge la Jamhuri ya Muungano lina Wabunge wa aina zifuatazo:

(i) Wabunge wa kuchaguliwa wanaowakilisha majimbo;

(ii) Wabunge wanawake wasiopungua asilimia 30% ya Wabunge wote wanaochaguliwa na vyama vya siasa kwa utaratibu wa uwiano wa kura;

(iii) Wabunge watano waliochaguliwa na Baraza la Wawakilishi Zanzibar angalau wawili wao wakiwa ni wanawake;

(iv) Mwanasheria Mkuu;

(v) Wabunge kumi walioteuliwa na Rais;

(vi) Spika endapo hakuchaguliwa kutokana na Wabunge.

**SIFA ZA WABUNGE**

Katiba inaweka sifa zifuatazo kwa wabunge:

(i) Awe raia wa Tanzania mwenye umri wa miaka 21 na ambaye anajua kusoma na kuandika katika lugha

ya Kiswahili au Kiingereza;

(ii) Awe ni mwanachama aliyependekezwa na chama chake;

(iii) Asiwe amepatikana na hatia mahakamani kwa kosa la kukwepa kodi ya Serikali katika kipindi cha miaka mitano kabla ya tarehe ya uchaguzi;

(iv) Asiwe amethibitishwa rasmi kuwa ni mgonjwa wa akili kwa mujibu wa sheria ya Jamhuri ya Muungano;

(v) Asiwe amepatikana na hatia na kupewa adhabu ya kifo na mahakama au kupatikana na hatia na kupewa adhabu ya kifungo cha miezi sita au zaidi kwa kosa la kutokuwa mwaminifu;

(vi) Asiwe amepatikana na hatia na kupewa adhabu na mahakama kwa kosa la utovu wa uaminifu au kuvunja maadili ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma;

(vii) Asiwe na maslahi yoyote katika mkataba wa Serikali wa aina yoyote aliyowekewa miiko maalumu kwa mujibu wa sheria na akakiuka miiko hiyo ;

(viii) Asiwe ameshika madaraka ya ofisa mwandamizi Serikalini, madaraka ambayo Rais haruhusiwi kumkabidhi Mbunge kwa mujibu wa Katiba hii au sheria ya Bunge ;

(ix) Asiwe amezuiliwa kupigiwa kura au kujiandikisha kupiga kura kutokana na ukiukaji wa Sheria za

uchaguzi wa Wabunge;

(x) Asiwe mgombea urais au Rais.

## MAISHA YA BUNGE

Bunge litafanya kazi zake kwa kipindi cha miaka mitano tangu kuitishwa kwake na Rais kwa mara ya kwanza. Hata hivyo Rais anayo mamlaka ya kulivunja Bunge kwa sababu mbali mbali ikiwa ni pamoja na:

a) Uhai wa Bunge kuisha;

b) Bunge kukataa kupitisha bajeti iliyopendekezwa na Serikali;

c) Ikiwa baada ya Muswada wa sheria kurejeshwa Bungeni na Rais, bado Wabunge watakataa kuubadili na kuurejesha tena kwa Rais auridhie, na Rais naye akataa kuuridhia;

d) Ikiwa Bunge limekataa kupitisha hoja ya Serikali na Rais haoni kuwa ufumbuzi ni kuteua Waziri Mkuu mpya;

e) Endapo kutokana na uwiano wa wingi wa Wabunge Rais haoni uhalali wa Serikali iliyopo kuendelea kubaki madarakani isipokuwa kuitisha uchaguzi mkuu.

## UCHAGUZI WA SPIKA

Spika ndiye kiongozi wa Bunge na atachaguliwa na Wabunge katika Kikao cha kwanza cha Bunge jipya kutoka miongoni mwa wananchi

wenye sifa za kuwa wabunge.

## HAKI NA KINGA ZA WABUNGE

Katiba imeweka na kulinda uhuru na haki ya wabunge kutoa mawazo Bungeni.

## TUME YA UCHAGUZI

Katiba ya Jamhuri ya Muungano imeunda Tume ya Uchaguzi yenye mamlaka ya kusimamia uchaguzi wa Rais wa Jamhuri, Wabunge wa Bunge la Jamhuri na pia madiwani. Sheria tatu hutumika kwa minajili ya kuendesha aina tatu za uchaguzi, Sheria ya Uchaguzi ya Jamhuri ya Muungano ya mwaka 1985 ambayo hushughulikia uchaguzi wa Rais wa Jamhuri na wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano, Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa ya Tanzania Bara na Sheria ya Uchaguzi Zanzibar ya mwaka 1984 kwa ajili ya uchaguzi wa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na madiwani Zanzibar.

Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na wajumbe wa Tume ya Uchaguzi ya Jamhuri ya Muungano wanateuliwa na Rais kutokana na watu wenye sifa zilizowekwa na Katiba kwa masharti kwamba ikiwa Mwenyekiti ameteuliwa kutoka Tanzania Bara basi Makamu Mwenyekiti atateuliwa kutoka Zanzibar na kinyume chake.

Tume ya Uchaguzi ya Jamhuri ya Muungano inao wajibu wa kusimamia shughuli zote za uchaguzi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano na pia Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano. Shughuli hizo ni pamoja na kugawanya majimbo ya uchaguzi na kuyatangaza, kuandaa na kusimamia uandikishwaji wa wapiga kura kwenye Daftari la Kudumu la wapiga kura, kusafisha au kurekebisha daftari hilo kila inapobidi ili kutoa fursa kwa wapiga

kura wapya kujiandikisha na waliofariki kuondolewa kwenye orodha ya wapiga kura, kuandaa na kusimamia utengenezaji wa karatasi za kupigia kura, fomu mbalimbali na vifaa vya kupigia kura, kuajiri wasimamizi wa uchaguzi na kutangaza washindi baada ya kura kuhesabiwa.



Jengo la Ofisi ya Tume ya Mabadiliko ya Katiba lililopo Mtaa wa Ohio, karibu na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Dar es Salaam.

## SURA YA NNE

## SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR, BARAZA LA MAPINDUZI ZANZIBAR, NA BARAZA LA WAWAKILISHI LA ZANZIBAR

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaundwa kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano na Katiba ya Zanzibar. Rais wa Zanzibar ndiye kiongozi na mkuu wa Serikali ya Mapinduzi na pia Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi la Zanzibar.

Rais wa Zanzibar huchaguliwa kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 na Sheria ya Uchaguzi ya Zanzibar ya mwaka 1984.

### BARAZA LA MAPINDUZI

Baraza la Mapinduzi ndilo Baraza la Mawaziri la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na wajibu wake ni kumshauri Rais wa Zanzibar kuhusu utekelezaji wa mambo yote yasiyo ya Muungano kuhusu Zanzibar.

### BARAZA LA WAWAKILISHI

Baraza la Wawakilishi la Zanzibar linao wajibu wa kutunga sheria za Zanzibar juu ya mambo yasiyo ya Muungano ya Zanzibar. Baraza la Wawakilishi lina sehemu mbili, sehemu ya Kwanza ikiwa ni Rais wa Zanzibar na sehemu ya pili ikiwa ni Wawakilishi.

## SURA YA TANO

## UTOAJI HAKI KATIKA JAMHURI YA MUUNGANO

Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano Mahakama ndicho chombo kikuu chenye mamlaka ya kutoa haki nchini. Mahakama ni muhimili huru wa dola ambao hauwezi kuingiliwa na mamlaka yoyote ya dola katika utendaji kazi wake.

Mahakama Kuu ya Jamhuri ya Muungano ndiyo yenye mamlaka makuu kuhusu utoaji haki Tanzania Bara juu ya mambo yote ya Muungano na mambo yote yasiyo ya Muungano kuhusu Tanzania Bara. Jaji Kiongozi wa Mahakama Kuu ya Jamhuri ya Muungano na majaji wengine wanateuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano baada ya kushauriana na Tume ya Utumishi wa Mahakama.

## MAHAKAMA KUU YA ZANZIBAR

Katiba ya Jamhuri ya Muungano inatambua kuundwa kwa Mahakama Kuu ya Zanzibar yenye mamlaka sambamba na Mahakama Kuu ya Jamhuri ya Muungano kwenye mambo yasiyo ya Muungano yanayoihusu Zanzibar. Katiba inaridhia kutungwa kwa sheria na Baraza la Wawakilishi Zanzibar kuunda mfumo wa kimahakama Zanzibar. Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 inaunda Mahakama Kuu ya Zanzibar na inaweka masharti ya kuteuliwa kwa Jaji Mkuu wa Zanzibar, Majaji wengine na utendaji kazi wao.

## MAHAKAMA YA RUFANI

Katiba ya Jamhuri ya Muungano inaunda Mahakama ya Rufani yenye mamlaka ya kusikiliza rufani kutoka Mahakama Kuu ya Jamhuri ya Muungano na Mahakama Kuu ya Zanzibar. Katiba ya

Zanzibar inazuia mambo kadhaa yasiletwe mbele ya mahakama ya Rufani ya Muungano kutoka Mahakama Kuu ya Zanzibar. Mambo hayo ni:

(a) Rufaa kuhusu Katiba ya Zanzibar;

(b) Mambo ya Kiislamu ambayo yameanzia katika Mahakama ya Kadhi;

(c) Jambo lolote jingine lililozuiliwa na sheria nyingine yoyote iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi.

Jaji Mkuu pamoja na Majaji wa Mahakama ya Rufaa wanateuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano. Masharti yao ya kazi na nidhamu ni kama yale ya Majaji wa Mahakama Kuu.

## MAHAKAMA MAALUMU YA KATIBA

Katiba ya Jamhuri ya Muungano inaunda Mahakama Maalumu ya Katiba yenye mamlaka ya kutatua migogoro ya kikatiba baina ya pande mbili za Muungano.

Mahakama hii ni ya usuluhishi na haina mamlaka ya kutengua maamuzi ya Mahakama Kuu wala Mahakama ya Rufani. Uamuzi wa Mahakama Maalumu ya Katiba hauwezi kukatiwa rufani kwenye Mahakama yoyote nchini. Majaji wa Mahakama hii wana uwiano wa nusu kwa nusu kutoka pande mbili za Muungano na huteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano.

## SURA YA SITA

## TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA NA SEKRETARIETI YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA

Katiba ya Jamhuri ya Muungano inaunda Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. Wajibu wa Tume hii ni kupokea malalamiko ya wananchi kuhusu uvunjwaji wa haki za binadamu nchini, kufungua mashauri mahakamani, kupinga uvunjwaji wa haki za binadamu na kurekebisha uvunjwaji huo, kufanya utafiti na kupeleleza ukiukwaji wa haki za binadamu na kuishauri Serikali kuhusu mambo yanayohusiana na haki za binadamu na utawala bora.



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Zanzibar Dkt. Ali Mohamed Shein, viongozi wa kitaifa katika picha ya pamoja na wajumbe wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba Ikulu, Dar es Salaam.

## SURA YA SABA

## MASHARTI KUHUSU FEDHA ZA JAMHURI YA MUUNGANO

Katiba ya Jamhuri ya Muungano inaunda Akaunti ya Fedha ya Pamoja ya pande mbili za Muungano. Akaunti hii ni sehemu ya Mfuko Mkuu wa Hazina ya Jamhuri ya Muungano. Fedha inayowekwa kwenye akaunti hii ni michango ya kila upande wa Muungano kwa matumizi ya mambo ya Muungano ya Jamhuri ya Muungano kama ilivyokubaliwa na pande zote mbili. Katiba inaunda Tume ya Pamoja ya Fedha na kuipa majukumu ya kusimamia mambo yote yahusuyo fedha ya Jamhuri ya Muungano.



Rais Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, akiwa katika picha ya pamoja na wajumbe wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba pamoja na viongozi wa Wizara ya Katiba na Sheria alipotembelea Ofisi ya Tume hiyo jijini Dar es Salaam.

SURA YA NANE

## MADARAKA YA UMMA

Kuundwa kwa Serikali za Mitaa Tanzania Bara na Zanzibar kumetambuliwa na katiba ya Jamhuri ya Muungano na kuwekewa lengo lake ambalo ni kupeleka madaraka kwa wananchi walipo, kijiografia na kiutawala ili wajiamulie mambo yanayohusu maendeleo yao wenyewe.



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, akiongea na mjumbe wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba Prof. Mwesiga Baregu nje ya Ofisi ya Tume.

## SURA YA TISA

### MAJESHI YA ULINZI

Masuala ya Ulinzi na Usalama wa Jamhuri ya Muungano yamewekewa masharti ya kikatiba na ni marufuku mtu au kikundi chochote kuanzisha au kuweka majeshi ya aina yoyote isipokuwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano.

Ni marufuku kwa wanajeshi kujiunga na chama cha siasa. Mamlaka ya kuongoza majeshi yamewekwa mikononi mwa Rais wa Jamhuri ya Muungano ambaye ndiye Amiri Jeshi Mkuu.

## SURA YA KUMI

### MENGINEYO.

Sura hii imeweka tafsiri ya misemo, istilahi na misamiati kama ilivyotumika kwenye ibara mbalimbali za Katiba.




Katibu Mkuu Kiongozi Balozi Ombeni Sefue akimkabidhi funguo za Jengo la Ofisi Mwenyekiti wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba Jaji Mstaafu Joseph S. Warioba, katika hafla fupi iliyofanyika Dar es Salaam.

# ELIMU KUHUSU  SHERIA YA MABADILIKO YA KATIBA, SURA YA 83 (KWA LUGHA NYEPESI)

## ELIMU KUHUSU SHERIA YA MABADILIKO YA KATIBA, SURA YA 83 (KWA LUGHA NYEPESI)

**UTANGULIZI:**

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ina lengo la kuwa imepata Katiba Mpya ifikapo mwezi wa Aprili, 2014 mnasaba na maadhimisho ya Miaka 50 ya Muungano wa Tanzania uliofanywa baina ya Zanzibar na Tanganyika Aprili 26, 1964.

Ili kulifikia lengo hilo imekubalika kuwa nchi ipitie katika mchakato wa katiba ili kuweza kupata maoni, matakwa na mahitaji ya umma ambayo ndio yatakayorutubisha uundwaji wa Katiba Mpya.

Mchakato huu unafanyika nchini kwa mara ya kwanza, na katika kufanikisha dhamira hiyo Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania limepitisha Sheria ya Mabadiliko ya Katiba, Sura ya 83, Toleo la 2012 ambayo inaainisha taratibu mbali mbali za kufikia lengo hilo.

Mchakato huu ni wa Watanzania, kwa maana ya umma wa Watanzania ambao ndiyo wenye mamlaka ya kushiriki mchakato huu kwa upana mkubwa na hatimaye kuamua juu ya Katiba Mpya.

Maeneo makuu ya Sheria ni kama yafuatayo:

a) **Madhumuni (Kifungu cha 4):**

Madhumuni ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ni kama yafuatavyo:

(i) Kuweka utaratibu wa kuunda Tume itakayo ratibu na kukusanya maoni ya wananchi

(ii) Kuweka utaratibu ambao utaruhusu wananchi kushiriki kwa uwazi na kwa mapana katika kutoa na kuwasilisha maoni yao kuhusu Katiba;

(iii) Kuweka utaratibu utakaowezesha kujenga muafaka wa kitaifa katika masuala yenye maslahi kwa taifa wakati wa mchakato wa Katiba;

(iv) Kuweka mfumo wa kisheria utakaowezesha kupiga kura ya maoni;

(v) Kuweka utaratibu wa namna ambavyo Katiba Mpya itakavyozinduliwa.

**b) Muda wa Mchakato (kifungu cha 8(1)):**

(i) Muda wa Mchakato utakuwa ni miezi 18;

(ii) Sheria inaruhusu kuongezwa miezi miwili iwapo itahitajika.

**c) Hatua za Mchakato:**

Kutakuwa na hatua zifuatazo hadi kupatikana kwa Katiba Mpya:

(i) Kuundwa Tume;

(ii) Utoaji wa Elimu ya Umma;

(iii) Ukusanyaji maoni;

(iv) Uchambuzi wa maoni;

(v) Uandikaji wa Rasimu ya Katiba;

(vi) Rasimu ya Katiba kujadiliwa katika Mabaraza ya Katiba;

(vii) Urutubishaji wa Rasimu baada ya michango katika Mabaraza ya Katiba;

(Viii) Bunge la Katiba kujadili Rasimu ya Katiba;

(ix) Kura ya Maoni;

(x) Kuanza kutumika kwa Katiba Mpya;

**d) Uundwaji wa Tume (kifungu cha 5, 6 na 7):**

(i) Inaundwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano kwa kushirikiana na kukubaliana na Rais wa Zanzibar;

(ii) Yamewekwa maeneo ya kuzingatiwa katika kufanya uteuzi huo ambayo ni pamoja na mteuliwa kuwa na sifa ya:

- kitaaluma
- kujali jiografia na mtawanyiko wa watu,
- umri
- uwakilishi wa makundi mbalimbali
- uaminifu na tabia isiyotiliwa shaka na jamii

- raia wa Tanzania

(iii) Muundo kamili wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba ni kama ufuatavyo

- Mwenyekiti.
- Makamo Mwenyekiti.
- Wajumbe 30 wakiwa ni 15 kutoka kila upande wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
- Katibu.
- Naibu Katibu.
- Sekretariati.

**d) Utoaji wa Elimu (kifungu cha 17(2)(a):**

Kwa kuwa utoaji wa elimu ya umma ni jambo muhimu katika mchakato huu wa kupata Katiba Mpya umewekewa utaratibu wake ambapo Tume ya Mabadiliko ya Katiba ndio yenye jukumu la awali katika wajibu huo wa kutoa elimu.

Sheria inafafanua juu ya utoaji wa elimu ya umma ya mabadiliko ya Katiba inayotambulika na Tume kwa mtu binafsi, taasisi, jumuiya au kikundi chengine chochote cha watu wenye malengo yanayofanana.

(i) Sheria inataka mtu binafsi, taasisi, jumuiya au kikundi chochote cha watu wenye malengo yanayofanana

kutuo taarifa kwa maandishi kwa Tume au kwa niaba yake kupitia:

- Mkuu wa Wilaya.
- Mkurugenzi wa Serikali ya Mitaa.
- Mkurugenzi wa Manispaa.
- Katibu wa Baraza la Mji au Wilaya.

(ii) Taasisi, jumuiya au kikundi cha watu wenye malengo yanayofana na ambacho lazima kiwe kimesajiliwa, wakati wa kutoa taarifa ya kutaka kutoa elimu, italazimu pia kutoa taarifa zifuatazo:

- Maelezo yanayohusu chanzo cha fedha za kuendeshea programu.
- Muda wa shughuli yake.
- Tarehe.
- Mahali.
- Eneo.
- Aina ya mada ya programu ya elimu itayotolewa.

(iii) Sharti la kutoa taarifa ya kuendesha programu ya elimu ya umma kwa kupitia Mkuu wa Wilaya, Mkurugenzi wa Serikali za Mitaa au Mkurugenzi wa

Manispaa, Katibu wa Baraza la Mji au Wilaya hakutakuwa ni sababu ya kuzuiliwa mtoa taarifa isipokuwa kwa sababu zitazoelezwa wazi kwa mtoa taarifa na Tume kuarifiwa.

iv) Jumuia, taasisi yaweza kuandaa mikutano kuwezesha wanachama wao kutoa maoni na kuwasilisha kwa Tume.

v) Jumuia au taasisi katika kufanya mikusanyiko ya hadhara itatoa taarifa kwenye mamlaka husika kwa kuzingatia sheria zinazosimamia uendeshaji wa mikutano au mikusanyiko hiyo.

**e) Hadidu za Rejea (vifungu vya 9, 17,18, 19 na 20):**

Hadidu za Rejea au Majukumu ya Tume ya Mabadiliko ya Katiba yametajwa katika vifungu mbali mbali kwenye Sheria. Hadidu Rejea hizo ni kama ifuatavyo:

(i) Kuratibu na kukusanya maoni;

(ii) Kupitia na kutafiti usahihi na ulinganifu wa masharti ya kikatiba yanayohusu mamlaka ya wananchi, mifumo ya kisiasa, demokrasia, utawala wa sheria na utawala bora;

(iii) Kutoa mapendekezo kwa kila hadidu za rejea;

(iv) Kuandaa na kuwasilisha ripoti;

(v) Kuandaa na kuendesha programu za kuelimisha juu ya madhumuni na majukumu ya Tume;

(vi) Kuitisha na kusimamia mikutano au mabaraza katika sehemu na nyakati mbali mbali.

(vii) Kutathmini na kuchambua kwa kutofautisha maoni ya wananchi yanayokubaliana na yale yaiyokubaiana.

(viii) Kuunda Mabaraza ya Katiba.

(ix) Kutengeneza Rasimu ya Katiba.

(x) Kuwasilisha Rasimu ya Katiba katika Bunge Maalum.

**f) Misingi ya kitaifa na maadili (kifungu cha 9(2):**

Tume itaongozwa na misingi mikuu ya kitaifa na maadili ya jamii ya kuhifadhi na kudumisha mambo yafuatayo:

(i) Kuwepo kwa Jamhuri ya Muungano;

(ii) Uwepo wa Serikali, Bunge na Mahakama;

(iii) Mfumo wa kiutawala wa kijamhuri;

(iv) Uwepo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar

(v) Umoja wa kitaifa, amani na utulivu;

(vi) Uchaguzi wa kidemokrasia kwa vipindi vilivyowekwa;

(vii) Ukuzaji na uhifadhi wa haki za binaadamu;

(viii) Utu, usawa mbele ya sheria na mwenendo wa sheria;

(ix) Uwepo wa Jamhuri ya Muungano isiyofungamana na dini yoyote na inayo heshimu uhuru wa kuabudu.

**g) Njia za kutoa maoni (vifungu vya 17, 18 na 22):**

Tume imepewa njia kadhaa za kupata maoni ya wananchi zikiwa zile kuu lakini nyengine ndogo ndogo mbali mbali. Njia hizo ni pamoja na zifuatazo:

(i) Kupitia ukusanyaji wa maoni;

(ii) Kupitia Mabaraza ya Katiba;

(iii) Kupitia Bunge Maalum;

(iv) Kupitia njia nyingine mbali mbali kama kuonana na watu, kuandikiwa Tume kwa njia mbalimbali.

**h) Bunge Maalum(kifungu cha 22):**

Baada ya hatua ya ukusanyaji wa maoni, kutengeza Rasimu ya Katiba, kuipeleka Rasimu hiyo katika Mabaraza ya Katiba na kurudi kuifanyia marekebisho, hatua itayofuata itakuwa Rasimu ya Katiba kupelekwa katika Bunge Maalum ambalo linatajwa katika Sehemu ya Tano ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba.

Rais ndie ataeitisha Bunge hilo ambalo wajumbe wake wameshaelezwa katika Sheria ya Mabadiliko ya Katiba na mamlaka ya Bunge Maalum yanatajwa katika Kifungu cha 25 nayo ni:

(i) Kujadiliana kupitisha masharti ya Katiba

inayopendekezwa;

(ii) Kutunga masharti ya mpito;

(iii) Kutunga masharti yatokanayo kama Bunge litavyoona inafaa.

Uamuzi katika Bunge Maalum utafikiwa kwa njia ya kura na kuhitaji kuungwa mkono kwa wingi wa theluthi mbili ya idadi ya wajumbe wote wa Bunge Maalum kutoka Tanzania Bara na theluthi mbili ya wajumbe wote wa Bunge Maalum kutoka Zanzibar.

Bunge Maalum litamaliza uhai wake baada ya kupitishwa kwa Katiba Mpya, ingawa Rais anawezakuliiitisha tena kwa kazi ya kuboresha masharti yaliomo kwenye Katiba inayopendekezwa.

**i) Bunge Maalum litakuwa na wajumbe wafuatao (kifungu cha 22(1)):**

(i) Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano;

(ii) Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar;

(iii) Wajumbe 166 watakaoteuliwa kutoka: asasi zisizo za kiserikali, asasi za kidini, vyama vya siasa vilivyo na usajili wa kudumu, taasisi za elimu ya juu, makundi yenye mahitaji maalum, vyama vya wafanyakazi, vyama vya wakulima, jumuia za wafugaji na makundi mengine.

**j) Kura ya Maoni(vifungu vya 31 mpaka 36):**

Sheria inaweka masharti ya Kura ya Maoni kwa madhumuni ya kuyapatia uhalali masharti yaliomo kwenye Katiba iliyopendekezwa na kupitishwa na Bunge Maalum.

Kura ya Maoni itaendeshwa na kusimamiwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa kushirikiana na Tume ya Uchaguzi wa Zanzibar, na kila moja ikisimamia upande mmoja wa Jamhuri ya Muungano ila matokeo yote yatatangazwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi .

Kutakuwa na swali moja litaloulizwa katika Kura ya Maoni ambapo mpiga kura atatakiwa ajibu NDIYO au HAPANA na matokeo ya kura hiyo yataamuliwa kwa kuungwa mkono kwa aasilimia inayozidi hamsini ya jumla ya kura zote zilizopigwa Tanzania Bara na asilimia inayozidi hamsini ya jumla ya kura zote zilizopigwa kutoka Zanzibar.

Iwapo Kura ya Maoni haikupita, Sheria inatoa fursa ya kurudiwa na iwapo wingi wa kura utakuwa ni HAPANA Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya mwaka 1977, itaendelea kutumika.

Mtu yeyote atakuwa na haki ya kupiga Kura ya Maoni iwapo jina lake limeingizwa katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura chini ya Sheria ya  Taifa ya Uchaguzi na Sheria ya Uchaguzi ya Zanzibar, isipokuwa kama amezuwiwa kupiga kura na sheria nyengine.

**k) Makosa (kifungu cha 21):**

a) Kifungu cha adhabu mbali mbali chini ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ni cha 21 na makosa yalioainishwa ni kama yafutayo:

(i) Kwa makusudi kukwamisha, kuzuia au kuchochea kwa vitendo au kuzuia kutenda kiasi cha Mjumbe, Tume au Sekretarieti kuathirika kutekeleza majukumu au mamlaka ya Tume;

(ii) Au kukwamisha, kuzuia au kuchochea mtu au kundi kutoa maoni kwenye Tume.

b) Makosa mengine ni (kifungu cha 21(1) na (2)) :

(i) Kukusanya maoni kinyume na Sheria hii;

(ii) Kujifanya mjumbe wa Tume au Sekretarieti;

(iii) Kuendesha programu ya elimu juu ya mabadiliko ya katiba kinyume na Sheria hii.

c) Adhabu inayotolewa kwa makosa chini ya sheria ni kwa mkosa kuwajibika kulipa faini ya Shs milioni mbili na isiyozidi milioni tano au kifungo cha mwaka mmoja na kutozidi miaka mitatu au adhabu zote mbili.

**l) Kuzinduliwa kwa Katiba na kumalizika kwa nguvu za Sheria hii (kifungu cha 38):**

(i) Katiba itakayopitishwa na Bunge Maalum na kuthibitishwa kwa Kura ya Maoni, itaaanza kutumika kwa tarehe itakayo kwenye Katiba hiyo;

(ii) Itazinduliwa na Rais;

(iii) Kuzinduliwa kwa Katiba Mpya kutaifanya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba kumaliza matumizi yake.




Ofisi Ndogo ya Tume ya Mabadiliko ya Katiba iliyopo katika jengo la Mfuko wa Barabara - Zanzibar.



Waziri Mkuu Mhe. Mizengo Pinda (Mb) akiongea na Mwenyekiti wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba nje ya Ofisi ya Tume Jijini Dar es Salaam.



Makamu wa Kwanza wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar Mhe. Seif Sharif Hamad akiongea na wajumbe wa  Tume ya Mabadiliko ya Katiba alipotembelea Ofisi za Tume Dar es Salaam.